HALMASHAURI YA WILWYA YA SENGEREMA

HOTOBA YA MWENYEKITI KWA WAHESHIMIWA MADIWANI WA HALMASHAURI YA SENGEREMA.

Mhe Mkuu wa Wilaya,

Katibu Tawala Wilaya,

Mhe mbunge,

Makamu mwenyekiti,

Wahe Madiwani,

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,

Wakuu wa Idara na Vitengo,

Wananchi

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali ya yote namshukru mungu aliyetujalia afya njema na kutukutanisha sote siku ya leo na aliyetuongoza kumaliza salama mwaka huu wa fedha 2022/2023, mwaka ambao tunajivunia kutekeleza malengo yetu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa mafanikio ya hali ya juu.

1.0 UTANGULIZI.

Waheshimiwa madiwani na wajumbe wote katika utekelezaji wa mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ilijiwekea malengo makuu Manne ili kuboresha na kutatua changamoto za kiuchumi zinazoikabili Halmashauri malengo haya ni kama yafuatayo:-

- Kuboresha ustawi wa jamii kupitia utawala bora na kutoa huduma bora na za kiwango kwa wannchi.
- Kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani Pamoja na kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani
- Kuimarisha usimamiaji na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo

- Kuboresha utekelezaji wa miradi ya Elimu, Afya, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na kuwezesha wananchi kiuchumi katika ngazi ya Msingi/Jamii kwa kushirikiana na wananchi.

2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema imekadiriwa kukusanya/kupokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni Hamsini na tano, milioni mia na tano na laki saba na tatu (55,505,703,000,.00) kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali. Ambapo mapato ya ndani ni shilingi biliono mbili na milioni miasaba na (2,750,000,000.00) Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ni Shilingi Bilioni moja miliono mia kumi na natano na Hamsini laki moja na sita (1,115,106,000) Ruzuku ya Mishahara ni Shilingi Bilioni thelathini na nane milioni miatano themeni na tatu na laki mbili na stinni (38,583,265,000.00) Pamoja na ruzuku ya Miradi ya maendeleo ambayo ni bilioni kumi na tatu na milioni Hamsini na saba laki tatu thelathininna mili (38,057,332,000)

Mapato ukilinganisha na Makisio ya mwaka

Hadi kufikia Juni 2023 Halmashauri imekusanya na kupokea Jumla ya Tshs. 56,406,632,895.70 ikiwa ni sawa na asilimia 91.44 ya lengo. Hadi kufikia mwezi Juni Halmashauri ilikukusanya na kupokea jumla ya Tshs.61,687,014,867.30 ikiwa Tshs. 55,505,703,000.00 ni bajeti iliyoidhinishwa na Tshs. 6,181,311,867.30 ni fedha iliyokuja nje ya bajeti kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya ndani na Serikali kuu bila bakaa.

Aidha Halmashauri imepokea Tshs. 3,040,000,000 ikiwa ni fedha za madarasa Kidato cha kwanza, Tshs.2,690,811,867.30 ikiwa ni fedha za WASH na Tshs. 450,500,000.00 ikiwa ni fedha za ujenzi wa shule zilizopatwa na majanga.

Kwa upande wa makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ililenga kukusanya Jumla ya Tshs. 2,750,000,000.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani. Hadi kufikia mwezi Juni Halmashauri imefanikiwa kukusanya Jumla ya Tshs. 2,158,371,403.33 sawa na 78.49% ya lengo.

Ambapo lengo la kukusanya mapato yasiyolindwa ni Tshs 2,043,228,000.00 Hadi kufikia Mwezi Juni Halmashauri imefanikiwa kukusanya Jumla ya Tshs 1,788,166,137,15 sawa asilimia 87.52 ya lengo.

Aidha Halimashauri ililenga Kukusanya Jumla ya Tshs 706,772,000.00 kupitia mapato lindwa, Hadi kufikia mwezi Juni Halmashauri imefanikiwa kukusanya Jumla ya Tshs 370,205,260.18 sawa na asilimia 52.8 ya lengo.

Mafanikio katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Ili kuboresha ustawi wa jamii na uchumi na kutimiza malengo ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imefanikiwa kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma katika sekta za Elimu ya Awali na Msingi Pamoja na Elimu ya Sekondari, Sekta ya Afya, uzoaji wa taka, miundombinu ya kilimo na mifugo Pamoja na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi Ambapo jumla ya miradi 53 yenye thamani ya Tshs 15,285,194,411.08 imetekelezwa kwa mchanganuo ufuatao;

- Mapato ya Ndani Tshs 573,300,000.00
- Mapato ya Nje Tshs 7,448,915,467.08
- Mapato toka Serikali kuu Tshs 2,538,374,000
- Nje ya Bajeti Tshs 4,724,604,944.00

Ufuatiliaji na Usimamizi wa Miradi ya Maendleo kupitia Kamati ya fedha

- Kupitia Kamati ya Fedha, Halmashauri imefanikiwa kuzuia matumizi ya fedha mbichi, ambapo kwa sasa hakuna matumizi ya fedha mbichi hela zote zinazokusanywa zinapelekwa benki na zinatumika kwa kufuata mpango wa Bajeti.
- Aidha kupitia uchambuzi wa Zabuni za Ujenzi wa wodi tatu na Mochwari katika katika Hospital ya Wilaya Mwabaluhi tumefaikiwa kuokoa Jumla ya Tshs. 100,000,000.00 ambapo Tshs 90,000,000.00 zimetumika katika ukamilishaji wa Jengo la Utawala na Tshs 10,000,000.00 kupangiwa matumizi mengine.

Ukarabati wa mtambo wa Halmashauri

Mtambo ni mzima na ratiba imetolewa kuanzia mwezi wa nane utaanza kufanya kazi ya kuchonga Barabara za ziizopo kwenye kata

Kitengo cha Taka Ngumu na Usafishaji.

Halmashauri imeboresha kitengo cha taka ngumu kwa kununua vifaa vya usafi, ukarabati wa trekta 2 pamoja na ukarabati wa vyoo 2 vya masoko ya soko kuu na soko la migombani.

Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

- Kupitia Idara ya Kilimo Halmashauri imefanikiwa kuboresha miudombinu ya Kilimo ambapo Ujenzi wa Mradi wa umwagiliaji Katungulu wenye ya Tshs 4,598,267,600.00 umeanza kutekelezwa tokea Januari 2023 na unatarajia kukamilika Juni 2024.
- Aidha Kupitia Idara ya kilimo kuna jumla ya Majosho manne yanaendelea kujengwa yenye thamani ya Tshs 92,000,000.00
- Uthibiti wa uvuvi haramu ambapo jumla ya Doria 24 zimefanyika na tumefanikiwa kuteketeza kokoro 84, Timba 102 na nyavu za dagaa mm8 nyavu 18.

Sekta ya Maendeleo ya Jamii

- Halmashauri imefanikiwa kutoa Mikopo kwa vikundi vya wanawake Vijana na Watu wenye ulemavu kiasi cha Tshs 124,000,000/=
- Idara imefanikiwa kusajili vikundi vya Kijamii CBOs 131.

Sekta ya Afya

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Sekta ya Afya imefanikiwa katika mambo yafuatayo.

- Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vituo 48 mwaka 2022 hadi vituo 53 mwaka 2023.
- Uimarishaji wa Miundombinu ya maji na usafi wa mazingira katika Vituo kutoka Vituo 13 mwaka 2022 Hdi vituo 39 mwaka 2023.
- Ongezeko la ujenzi wa majengo ya kutolea huduma katika hospital ya Wilaya toka majengo 8 .mwaka 2022 hadi majengo 12 mwaka 2023-08-17.
- Kuanza kwa huduma za awali katika Hospital mpya ya Wilaya (Mwabaluhi).
- Ukamilishaji wa maboma ya Zahanati katika Vijiji vya Buyagu, Nyitundu na Lugongo.

- Ufunguzi wa Zahanati mbili mpya za Mami na Ishishang'holo.
- Mapokezi ya Watumishi wapya 24.
- Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 16 mwaka 2022 hadi vifo 08 mwaka 2023.

Sekta ya Elimu ya Awali na Msingi

- Kuongozeka miundombinu katika Shule za Awali na Msingi kutoka mvymba vya madarasa 996 kwa mwaka 2021/2022 hadi vyumba vya madarasa 1,080 kwa mwaka 2022/2023 ambalo ni ongezeko la vyumba vya madarasa 84.

- Kuongezeka kwa madawati kutoka madawati 22,209 kwa mwaka 2021/2022 hadi madawati 23,309 kwa mwaka 2022/2023
- Kuongezeka kwa matundu ya vyoo kutoka matundu 1,696 kwa mwaka 2021/2022 hadi matundu 1881 kwa mwaka 2022/2023.

- Kuongezeka kwa ufaulu Mtihani Darasa la saba kutoka asilimia 76% kwa mwaka 2021 hadi asilimia 77.1% kwa mwaka 2022.

- Ujenzi wa Nyumba 4 za Walimu zimejengwa na zimekamilika.

Sekta ya Elimu Sekondari

- Halmashauri kupitia Idara ya Elimu Sekondari imefanikiwa kuongeza miundombinu na kufundishia ambapo kwa mwaka 2022/2023 jumla ya vyumba vya Madarasa 152, vimejengwa Nyumba za walimu 2 zimejengwa Ujenzi Daharia 1 katika Shule ya Sekondari Nyamatongo ambapo ujenzi bado unaendelea.
- Usajili wa Shule mpya ya Sekondari Ibondo
- Tumefanikiwa kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa ambapo kwa mwaka 2022 ufaulu ulikuwa 88% kwa wanafunzi wa kidato cha pili na kidato cha nne ufaulu ni aslimia 89% na kidato cha Sita Ufaulu ni asilimia 100%

Sekta ya Utumishi na Utawala

- Halmashauri imefanikiwa kupandisha madaraja. watumishi wapatao 1,291.
- Halmashauri imeajiri Watumishi 237 katika idara mbalimbali za Halmashauri.
- Vikao vyote vya Kisheria vimefanyika bila kukosa, kwa mujibu wa Sheria na taratibu na ushauri wa wataalamu umezingatiwa na kufanyiwa kazi.

Changamoto

Katika kila mafanikio hapakosi changamoto mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imekabiliana na kuu mbili katika utekelezaji wa bajeti.

- Upungufu vymba vya madarasa na matundu ya vyoo katika Shule za Msingi na Sekondari na hili ni kutokana na Elimu bila malipo ambapo Jamii imehamasika kupeleka Watoto shule.
- Mwamko mdogo wa wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (iCHF)

Mpango na Bajeti Kwa mwaka fedha 2023/2024

Kwa kawaida utekelezaji wa Malengo na utatuzi wa changamoto za Halmashauri zinaongozwa na mpango mkakati wa Halmashauri,hivyo tunaendelea kutimiza malengo kama yalivyo kwenye Mpango mkakati wa Halmashauri na katika Mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri imepanga kutekeleza Mpango na bajeti wenye thamani ya Tshs 53,234,555,000.00 ambapo Tshs 35,664,176,000.00 ni fedha za mishahara ya watumishi, Tshs 1,115,111,000.00 ni kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali kuu, Tshs 13,441,178,445.00 ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Tshs 2,535,742,555.00 ni fedha za mapato ya ndani ambapo mapato lindwa ni Tshs 400,750,000.00 na Tshs 78,000,000.00 ni fedha kwa ajili ya Ngazi za chini (Kata na Vijiji)

HITIMISHO

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Wahemishiwa Madiwani na Wataalam wa Halmashauri ya Sengerema, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimwa Dr. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha Serikali na wadau wa Maendeleo kutoa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kiwango cha juu ambacho kimewezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kufanyika bila kutegemea nguvu za wananchi kwa kiasi kikubwa. Aidha miradi husika itasaidia kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi katika Wilaya, Mkoa na Serikali kwa ujumla.

Shukrani hizi pia ziwaendee wafuatao

- Kamati za Fedha, Uongozi na Mipango
- Kamati ya Uchumi na Mazingira
- Kamati ya Elimu, Afya na Maji
- Kamati ya menejiment (CMT)

Kwa ufuatiliaji na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo imefanyika kwa ubora unaostahili.

Naomba kuwasilisha.

Mh. Yanga E. Makaga
MWENYEKITI WA HALMASHAURI (W)
SENGEREMA